**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA TANO

**11 APRILI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA TANO – TAREHE 11 APRILI, 2017

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**35. MHESHIMIWA LAMECK OKAMBO AIRO (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Kata ya Koryo kwa kushirikiana na Mbunge wao na Wananchi wa Rorya wanaoishi Mwanza, Arusha na Dar es Salaam wamejenga wodi ya akinamama na watoto pamoja na kununua jokofu lakini mapungufu yaliyopo sasa ni jengo la upasuaji:-

Je, Serikali sasa haioni ipo haja ya kusaidia jengo hilo pamoja na vifaa vyake.

**36. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Kyerwa yamewekwa katika Kata ya Kyerwa:-

Je, ni mchakato gani ulifanyika mpaka Kata ya Kyerwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya.

**37. MHESHIMIWA QAMBALO WILLY QULWI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Karatu ina umri wa zaidi ya miaka 20 lakini bado haina Hospitali ya Wilaya jambo ambalo linawatesa wakazi wengi hasa wazee, akinamama na watoto:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Kituo cha Afya cha Karatu kuwa Hospitali ya Wilaya.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**38. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Biashara ya vyuma chakavu imeshamiri sana Tanzania Bara na

Visiwani na imesababisha madhara ya kuharibiwa na kuibiwa kwa miundombinu mbalimbali ikiwemo mifuniko ya chemba za maji taka:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kupambana na wizi na uharibifu huo wa mali za Serikali na wakati mwingine walinzi wa maeneo husika wanashuhudia hayo;

(b) Je, Serikali haioni kwamba hata usalama wa raia na mali zao pia uko mashakani.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**39. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege katika eneo lililotengwa katika Kijiji cha Manga kwa msaada wa Benki ya Dunia.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**40. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kujenga mradi wa maji wa Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao.

**41. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-Wananchi wa Kitere na Bonde la Mto Ruvuma wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha Mpunga kwa miaka mingi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima hao kuwa na kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**42. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Tanzania imekuwa ikipeleka vikosi vya kulinda amani ndani ya Afrika na

sehemu nyingine Duniani kadri mahitaji na hali inavyoruhusu na kutimiza dhima ya amani Duniani:-

(a) Je, mazoezi kama haya yanaimarisha jina la Tanzania kiasi gani katika jukumu hili;

(b) Je, katika miaka kumi iliyopita Tanzania imepeleka vikosi maeneo gani na kwa misingi gani;

(c) Je, changamoto gani zinakuwepo katika kukusanya vikosi hivyo kabla havijapelekwa nje ya nchi kwa kazi kama hizo.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

### 43. MHESHIMIWA MARGARETH SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kutatua matatizo ya Wakulima wa Tumbaku katika Mkoa wa Tabora wakiwemo wa Wilaya ya Urambo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda Bodi ya Tumbaku (TTB) nyingine ili ianze kazi haraka iwezekanavyo baada ya Bodi ya Tumbaku iliyovunjwa;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pembejeo za msimu ujao zinamfikia mkulima wa Tumbaku mapema wakati huu ambapo Bodi husika imevunjwa.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

**44. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Kuna Malalamiko makubwa kwa upande wa Zanzibar kuhusu Idadi ndogo ya Wanafunzi wanaopata Mkopo wa Elimu ya Juu, jambo ambalo linapunguza idadi ya Wataalamu kwa upande wa Zanzibar na hivyo kushindwa kuingia katika soko la ajira katika Afrika Mashariki na Kati na kuijenga Nchi yetu kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inatakiwa kutenga asilimia maalum kwa Wanafunzi kutoka Tanzania Zanzibar;

(b) Je, Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni kiasi gani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**11 APRILI, 2017** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA